

(A)

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA KUKODISHA GARI-FUSO KWA AJILI YA KUSAFIRISHA VIFAA VYA
UJENZI- VYOO, WHITE CEMENT, WAYA ZA UMEME

KWA AJILI YA UJENZI WA CHUO CHA VETA RUFIFI

MKATABA NA: PA/24/2021/2022/TRA/RUF-16

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 30 mwezi 03 - 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

M/S PASCHAL & SONS TRANSPORT COMMISION AGENT wa S. L. P.70981 DAR ES SALAAM. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa usafirishaji vifaa ") kwa upande mwengine.

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIFI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIFI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFIFI ambayo ujenzi wake unaendelea;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA ZA USAFIRISHAJI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania **1,600,000/=** kwa kuasafirisha vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam mpaka eneo la ujezi Utete Rufiji kama inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu,kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama za usafirishaji vifaa vya ujenzi"

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

S/N	STAGE	BEI ILIYOKUBALIKA
1	GHARAMA ZITAKAZOTUMIKA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI VILIVYOKUWA VINADAIWA KWA MZABUNI KUTOKA KAMAKA KWENDA ENEO LA UJENZI UTETE RUFIFI(VYOO,WHITE CEMENT,WAYA ZA UMEME)	1,600,000
JUMLA		1,600,000

2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI (TRANSPORTATION SUM ADJUSTMENT)

Gharama za usafirishaji hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Malipo yatafanyika baada ya kazi kukamilika yaani Mzigo kufika eneo la ujenzi ukiwa salama na kwa idadi na kiwango kilichotakiwa.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Mzabuni wa usafirishaji atakabidhi mzigo kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha uhalali wa mapokezi ya mzigo husika.

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni wa usafirishaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

5. WAJIBU WA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kusafirisha mzigo wa vifaa vya ujenzi kwa kadri alivyokubaliana katika mkataba sambamba na maelekezo ya Mwajiri.




IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA
PWANI (PWANI RVTSC)

Jina: CLARA KUBODYA Saini: 

Wadhifa: Kaimu Nkumu WACHE Tarehe: 30/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: LUKA C. MKINI Saini: 


Wadhifa: MKINI KAMANI
YA UZURU Tarehe: 30/03/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Jina: PASCAL RAINA Mbele ya 
Wadhifa: DIRECTOR Saini: 



Mbele ya (Shahidi)

Jina: JULIUS JONAS Saini: 

Wadhifa: SECRETARY Tarehe: 30/03/2022

